

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Anwani ya simu "AFYA", DAR ES SALAAM
Simu nambari: 255 22 2120261
(Barua zote ziandikwe kwa Katibu Mkuu)



6 Barabara ya Samora Machel,
S. L. P. 9083,
11478, DAR ES SALAAM.

Kumb. Na. CJB 300/620/01"/35

07 Septemba, 2016

Waganga Wakuu wa Mikoa, Wilaya,
Hospitali za Mashirika ya Dini na Binafsi
TANZANIA.

**YAH: TAARIFA YA KATAZO KWA WANAFUNZI WATARAJIWA WA UTABIBU
WANAOJIFUNZA KWA KUANGALIA KATIKA HOSPITALI HAPA NCHINI.**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

Wizara ya Afya.. Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inapenda kutoa taarifa hii kwa Waganga Wakuu wote wa Mikoa, Wilaya, Hospitali za Mashirika ya Dini na Binafsi nchini kufuatia kupata taarifa ya kuwepo kwa mikataba ya mafunzo baina ya Hospitali zetu hapa nchini na mashirika mbali mbali ya nje ya nchi ambayo wanaleta wanafunzi kufanya mafunzo kwa vitendo au kwa kuangalia shughuli zote zitolewazo mahospitalini kinyume na misingi ya taaluma na kanuni za Tiba.

Wizara imebaini haya yanafika kupitia barua yenyeye Kumb. Na. FA.207/251/01/65 ya tarehe 07/05/2010 yenyeye kichwa cha habari "**WANAFUNZI WA UTABIBU KUTOKA UNGEREZA, MAREKANI NA CHINA KUJIFUNZA KWA KUANGALIA KATIKA HOSPITALI YA MKOA WA IRINGA**", kwamba Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa sasa inatumika kwa ajili ya kutoa mafunzo "kwa njia ya kuangalia" kwa wasio wanafunzi wa vyuo vya kitabibu. Barua hiyo pia, imenakiliwa na kutumika kuingia mkataba na hospitali nyingine ikiwapo Hospitali ya Mkoa ya Morogoro. Hii ni kinyume na Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi na Miiko na Maadili ya kitaaluma. Ikumbukwe kwamba, wanaoruhusiwa kuangalia wakati huduma inatolewa kwa wagonjwa (observation for clinical practice) au kushiriki huduma ya kitabibu nchini Tanzania ni wafuatao:-

- Wanafunzi vyuo vya kitabibu vilivyosajiliwa na waliohitimu masomo ya kitabibu mafunzoni na hivyo wanaenda mahospitalini kupata mazoezi kwa vitendo..
- Wahitimu kamili toka vyuo vya kitabibu vilivyosajiliwa wanapokuwa mafunzo kwa vitendo au wanapokuwa tayari wamesajiliwa kufanya kazi za kitabibu.
- Wale wote waliohitimu fani husika na kupata usajili na mabaraza ya kitaaluma kwa fani husika nchini Tanzania.
- Maombi yote kwa wadau kutoka nje ya nchi lazima yapitie Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Balozi zao.

Aidha, barua tajwa hapo juu ilitolewa kwa ajili ya kipindi hicho cha Mei, 2010 kwa ajili ya hao walioombewa kipindi hicho na siyo kwa ajili ya matumizi endelevu kama inavyofanyika sasa. Na hata hivyo maombi hayo yalikuwa kwa wanafunzi wa utabibu ikimaanisha kuwa wanafunzi hao walikuwa wamejiunga na vyuo kadhaa vya utabibu nchini marekani, Uingereza na China na hivyo walikuwa wanakuja kwenye "Apprenticeship" au "Elective period" jambo ambalo ni la kawaida kwenye mafunzo. Badala yake imefahamika kuwa wanafunzi hao hawajajiunga na vyuo vyovoyote vya utabibu. Hivyo kwa barua hii, **nafuta barua hiyo yenye Kumb. Na. FA.207/251/01/65** ya tarehe **07/05/2010** yenye kichwa cha habari "**WANAFUNZI WA UTABIBU KUTOKA UINGEREZA, MAREKANI NA CHINA KUJIFUNZA KWA KUANGALIA KATIKA HOSPITALI YA MKOA WA IRINGA**".

Wizara inawaelekeza Waganga wakuu wote, kusitisha mara moja mafunzo hayo na kufuata taratibu zenu za kimkataba kusitisha mikataba hiyo kwani haikidhi Maadili ya kitaaluma na Sera za nchi yetu. Kwa wale wote wenye aina hiyo ya mafunzo watoe taarifa Wizarani baada ya kuchukua hatua stahiki. Kwa wale ambao tayari wamegunduliwa kuwa na mafunzo hayo wamepewa barua ya kuwaamuru kuyasitisha ndani ya siku saba (7) na kutoa taarifa.

Angalizo, hapa nchini tunawanafunzi wengi wanaohitaji kupata mafunzo kutumia hospitali zetu lakini hawapati nafasi za kutosha kwa maeleo ya kuwa hakuna watumishi na vifaa tiba vya kutosha, naelekeza pia kuwa wanafunzi wote halali wanaopata mafunzo katika hospitali zetu wapate usimamizi wa kutosha kwani ndicho kiapo cha utoaji huduma za Tiba kinavyoagiza na Waganga wakuu wote lazima msimamie. Aidha, unatakiwa kuhakikisha kuwa huduma za hospitali/vituo vya tiba zinatolewa kwa kuzingatia Miiko na Maadili ya Tanzania.

Nakutakia kazi njema.

Mpoki
Dkt. Mpoki M. Ulisubisya
KATIBU MKUU

Nakala:

- Katibu Mkuu,
OR TAMISEMI,
S.L.P. 1923.
DODOMA.
- Makatibu Tawala Mkoa,
- Mkurugenzi Mtendajji
CSSC
Tanzania
- Mkurugenzi mtendaji
APHTA
Tanzania